TANGAZO LA SERIKALI NA. 495 la tarehe 15/7/2022

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA 288)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 89

SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA UBUNGO, 2022

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Afya na Usimamizi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo za Mwaka 2022.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo: -

"Ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya Huduma, Vibali au Leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri

"Adha" maana yake ni hali yoyote mbaya yenye kuleta madhara juu ya afya ya watu kwa ujumla.

"Afya" maana yake ni hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii na wala sio tu kutokuwa na ugonjwa au ulemavu.

"Afya ya mazingira" maana yake ni sayansi ya afya ya umma inayoangalia mahusiano kati ya binadamu na mazingira anayoishi na kuboresha afya na utimilifu wa afya yake na kuwezesha jamii kuishi katika mazingira salama.

"Afisa Afya ya mazingira" ni afisa ambaye anashughulikia afya ya mazingira.

"Afisa Bustani" Ni Afisa aliyepewa dhamana ya kusimamia bustani maeneo ya wazi, mizunguko ya barabara (Round abouts), na maua yaliyo kati na kando ya barabara katika Halmashauri.

"Afisa Mazingira" Ni Afisa yoyote aliyepewa dhamana ya kusimamia mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004.

"Afisa Misitu" Afisa yeyote aliyepewa dhamana ya kusimamia Misitu, Miti, Bustani za Miti na Maua, na maeneo ya wazi katika Halmashauri.

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Umma atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa, hii ni pamoja na:-

(a) kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula;
(b) kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula;
(c) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula (binzari na vingine vinavyofanana na hivi);

"Chanzo cha maji" Ni eneo lolote ambalo limetunzwa kwa ajili kua chanzo cha maji (Catchment Area) kwa matumizi ya jamii.

"Choo cha kuvuta" maana yake ni choo ambacho kimejengwa na kuunganishwa na maji na kuwa na kifaa kinachoweza kusukuma maji kwa ajili ya kuondoa uchafu hadi mahali palipoandaliwa;

"Choo bora" maana yake ni choo chochote cha maji chenye sakafu inayosafishika, banda imara la kudumu, limeezekwa, lina mlango imara, bomba la kutolea hewa chafu na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwa kwa vifaa vya kudumu.

"Choo cha Umma" maana yake ni choo kilichojengwa na Halmashauri au wakala wake au mtu binafsi au kampuni kwa matumizi ya umma na kuthibitishwa na Halmashauri pamoja na baraza la afya la mazingira;

"Eneo la wazi" maana yake ni eneo lililo chini ya Halmashauri ambalo limekatazwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo;

"Hati ya usafi" maana yake ni hati itakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa inayothibitisha kukaguliwa kwa maeneo yote yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hizi kulingana na Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2012 na kanuni zake:

"Hifadhi ya Mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji kwa kuzingatia masharti na maelekezo ya Sheria ndogo hizi au sheria nyingine zinazohusu mazingira;

"Jengo la biashara" maana yake ni jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli za biashara;

"Kamati ya Mazingira" maana yake ni kamati iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi kusimamia shughuli za usafi wa mazingira;

"Kaya" maana yake ni familia ya watu akiwemo baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo, au watu wanaokaa katika nyumba moja au ndani ya chumba kimoja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba;

'Kelele" maana yake ni kero isababishwayo na sauti ambayo kwa asili inakataliwa au ile ambayo inaweza kusababisha athari mbaya kwa afya ya binadamu au mazingira, sauti ya aina hii pia inaweza kubainishwa na kamati ya taifa na viwango kwa mujibu wa sheria ya mazingira Na. 20 ya mwaka 2004.

"Kero au chukizo" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni kichafu kiasi cha kusababisha magonjwa kwa binadamu, kuhifadhi mbu, nzi, panya na viumbe wenye madhar vinavyoweza kusababisha: -

(a) Hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu.
(b) harufu mbaya na inayouudhi au kuleta kinyaa
(c) kuzaliana kwa wadudu na wanyama hatari kama vile inzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;

'Kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa sheria ndogo hizi.

"Kikundi cha Mazingira" maana yake ni kikundi chochote cha watu kilichosajiliwa kufanya usafi na usimamizi wa mazingira na udhibiti wa uharibifu

wa mazingira katika maeneo ya Halmashauri;

"Kikundi cha usafishaji" maana yake ni kikundi chochcote cha watu kilichosajiliwa kufanya usafi wa mazingira na hasa za udhibiti wa uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Halmashauri

"Kituo cha taka" maana yake ni eneo maalum lililowekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kuweka taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye dampo la taka ngumu la Halmashauri;

"Kituo cha maji machafu" maana yake ni sehemu maalumu iliyotengenezwa kwa ajili ya ukaguzi wa mfereji ambao una mfuniko usioruhusu hewa kutoka.

"Kizimba cha taka" ni eneo lililowekwa na Halmashauri kwa ajili ya kuhifadhi taka ngumu;

"Kuchakata Taka" maana yake ni kuchambua, kuzitenganisha, kuzibadilisha na kuwa kitu kingine au kutoa zao jingine lenye manufaa kwa jamii;

'Kuvuna Msitu' maana yake ni kufyeka, kukata au kung'oa miti au visiki.

"Mabwawa ya maji taka" maana ni yake mabwawa yaliyojengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi na kuchakata maji taka yaliyokwishatumika kwenye shughuli mbalimbali.

"Madini ya Ujenzi" Ni aina zote za madini ya ujenzi yaliyoainishwa katika Sheria ya Madini.

'Maeneo nyeti" maana yake ni maeneo oevu, mitelemko ya milima, misitu au maeneo maalumu yaliyotengwa kwa minajili ya misitu au bustani.

'Maji' maana yake ni kama ilivyotafsiliwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira, na ni pamoja na

maji ya kunywa ya mito, vijito, maji yanayotiririka, yaliyohifadhiwa, yaliyo katika visima, mabwawa, mifereji, madimbwi, maziwa, bahari, maji yaliyoko chini ya ardhi, na maji yaliyoko katika mkondo wa asili.

"Mazalio ya wadudu" maana yake ni mazingira ambayo wadudu huzaliana au kuishi kwa minajiri ya kufanya mzunguko wa maisha na baadae huleta madhara kwa binadamu na mazingira wanamoishi.

"Mazao ya misitu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya kifungu cha 2 cha sheria ya Misitu na ni pamoja na kitu chochote kinachopatikana au kuzalishwa pamoja na miti, mazao yanayoota kupatikana msituni, ambao ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito, mbao, mbegu za miti, nta, asali, utaa, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama, majani, mizizi, gundi, utomvu, maranda, matete, kamba, makuti (mawale), nyuzi za wanyama, mimea (miti) na kitu chochote chenye uhai au kisicho na uhai kitakachotangazwa katika gazeti la Serikali kuwa ni zao la misitu;

Sura ya 191

"Mazingira" maana yake ni masuala yote yanayohusisha maumbile halisi yawazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia ya nchi, sauti, mwanga, harufu, hali za kibaiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii za binadamu na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana.

"Mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anaejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri.

"Mgahawa wa nje ya jengo" maana yake ni

shughuli zote za uuzaji wa chakula na vinywaji zinazofanyika katika sehemu ya nje ya jengo maalum la mgahawa au hoteli

"Misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 na miti, uoto wa asili au uliopandwa, au asilimia 50 au zaidi ya vichaka na miti inayoota au ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya sheria za misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri.

"Mkaguzi wa Mazingira (Environmental Inspector)" Ni Afisa aliyepewa dhamana ya Ukaguzi wa Mazingira kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mazingira.

"Mifugo" maana yake ni wanyama wote wafugwao na binadamu kama vile mbwa, ng'ombe, punda, nguruwe, mbuzi, kondoo na kuku.

"Mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ubungo pamoja au Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mmiliki" maana yake ni mtu yeyote ambaye ana miliki ardhi, sehemu za starehe, nyumba za kulala wageni, nyumba za kuuzia vyakula, kumbi za starehe, mpangaji, wakala wa mpangishaji wa nyumba au jengo na makazi yoyote ndani ya eneo la Halmashauri;

"Mzalishaji wa taka ngumu" maana yake ni mtu yeyote, kaya, taasisi, biashara, kiwanda ambacho katika kutekeleza shughuli zake huzalisha taka

ngumu;

“Mtandao wa maji taka” maana yake ni mfumo wa bomba kuu lililijengwa kwa madhumuni ya kupokea na kusafirisha taka miminika toka kwenye mifereji ya maji na kuyapeleka kwenye mabwawa ya maji taka au baharini;

“Mzalishaji wa maji taka” maana yake ni mtu, shirika, kiwanda au taasisi ambapo shughuli zake huzalisha maji taka;

“Pipa la taka” maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira;

‘Rasilimali” maana yake ni kitu chochote cha asili au urithi, au hali yeyote katika Halmashauri.

“Rasilimali za Asili” maana yake ni kitu chochote cha asili (Urithi) au hali yoyote ile katika ardhi ya halmashauri chenye manufaa kiuchumi na kijamii.

“Taka” maana yake ni kitu chochote ambacho baada ya kukitumia hakina thamani kwa wakati huo na uwepo wake katika eneo hilo unaweza kusababisha chukizo la kiafya na kuhatarisha afya ya jamii;

“Majitaka” maana yake maji yaliyokwisha tumika au chafuliwa kwa namna yoyote ile ambayo yanajumuisha maji machafu toka chooni, bafuni, jikoni, viwandani, maji yaliyooshewayo vyombo, maji yaliyofuliwa nguo, kuosha nywele, kuoshea vyakula na yaliyopigiwa deki na kutoka kwenye taasisis mbalimbali;

“Taka Ngumu” maana yake ni aina zote za taka

zinazozalishwa majumbani, kwenye taasisi, maeneo ya biashaa na viwandani lakini hazihatashi majitaka au takahatashi;

‘‘Taka hatarishi’’ maana yake ni taka iliyotafsiriwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingia;

“Taka za Majumbani” maana yake ni mabaki ya chakula, maganda ya matunda, majivu, kinyesi cha mifugo, taka za bustani, nguo chakavu, karatasi za aina mbalimbali na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;

“Taka za Viwandani” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

“Tathmini ya athari kwa mazingira na kijamii” maana yake ni uchunguzi wa hatua unaofanywa kubaini iwapo programu, shughuli, au mradi utakuwa na madhara kwenye mazingira;

“Uchafu Hatari” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira;

“Uchunguzi wa Afya” maana yake ni hali ya mtu kupima afya yake kwa kuchukuliwa vipimo vya ndani na nje ya mwili ili kubaini kuwepo kwa vijidudu vya magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi;

“Ufugaji Endelevu” maana yake ufugaji unaofuata taratibu kwa mujibu wa sheria ya mifugo.

“Ufugaji wa ndani” maana yake ni ufugaji wa mifugo ndani ya nyumba, banda au zizi ndani ya eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;

“Ugonjwa wa kuambukiza” maana yake ni ugojwa wowote uambukizao kutoka kwa mtu na mtu au mtu kwa mnyama, mtu kwa mdudu mfano kifua

Tangazo serikali na. 495 (linaendelea)

Sura 191

kikuu, kimeta, safura, surua,kipindupindu, uti wa mgongo n.k

"Vitu hatari" maana yake ni vitu vyote vilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, ni pamoja na kemikali yoyote, taka gesi, madawa, vidonge, mimea, wanyama au viumbe au visivoonekana na ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu,maisha au mazingira;

Sura 191

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Wasaidizi wa Kutunza Mazingira (Street Environmental Volunteer)" maana yake ni pamoja na Askari JKT, askari wa jeshi la akiba (mgambo), Watu binafsi ambao wameteuliwa kusimamia shughuli za usafi na utunzaji wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi.

SEHEMU YA PILI
WAJIBU WA HALMASHAURI KATIKA USIMAMIZI WA AFYA, USAFI NA MAZINGIRA

Uwezo wa Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na uwezo wa;

(1) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za usafi afya na mazingira,

(2) Kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kufuata kanuni za afya, usafi na kutunza mazingira

(3) kuteua mtu yeyote, wakala, kikundi au Taasisi kutekeleza shughuli za usimamizi wa afya, usafi na mazingira kwa niaba ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi

(4) Kufanya ukaguzi ili kubaini endapo kanuni za afya, usafi na utunzaji wa mazingira zinazingatiwa ndani ya eneo la Halmashauri

(5) kumchukulia hatua za kisheria mtu yoyote anayekiuka Sheria Ndogo hizi au sheria nyingine inayohusiana na afya, usafi na usimamizi wa mazingira zilizotungwa na Bunge.

(6) Kutunga kanuni, miongozo au kutoa maelekezo yatakayosaidia kulinda Afya, usafi na Usimamizi wa Mazingira ndani ya eneo la Halmashauri

(7) Kuingia mkataba na mtu yeyote, taasisi au Kampuni kutelekeza shughuli za usimamizi wa afya, usafi na mazingira kwa niaba ya Halmshauri katika eneo ndani ya Halmashauri.

Ada ya Uzoaji taka

5 Halmashauri itatoza Ada ya taka katika kufanikisha utekelezaji wa Usimamizi wa Mazingira kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Uteuzi wa Wakala

6 Halmashauri ina mamlaka ya kuteua Wakala kukusanya Ada kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa Wakala

7. Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa: -

(a) Kukusanya Ada kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(b) Wakala atakusanya Ada kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

(c) Atekeleze yote yaliyomo kwenye mkataba.

SEHEMU YA TATU
USAFI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

8. (1) Ni wajibu wa kila mkazi au mfanyabiashara anayemiliki jengo au eneo la biashara kuhakikisha kwamba: -

(a) Majani yanayozunguka jengo lake au makazi yanakatwa au kupaliliwa katika eneo lote hadi mwanzo wa mipaka ya barabara ya mbele ya nyumba yake au eneo lake;

(b) Taka ngumu zote zinakusanywa, kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililopangwa na Halmashauri;

(c) Majitaka yanaelekezwa ndani ya mfumo wa majitaka (sewerage systeam).

(d) Ataboresha kwa kupaka rangi ya jengo lake kila inapochakaa.

(e) Atakuwa na choo kilicho bora na kisafi wakati wote.

(f) Anashiriki siku ya usafi ya Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi.

(g) Ataondoa uchafu ikiwemo mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo katika mifereji ya maji ya mvua inayomzunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mifereji hiyo inakuwa safi wakati wote.

(h) Ataweka taa yenye mwanga nje ya jengo analoishi au analolitumia kwa shughuli yoyote na atatakiwa kuiwasha wakati wa usiku.

(i) Kuhakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuathiri upitishaji wa maji ya mvua na hivyo kuruhusu kuwepo wa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye

madhara kwa afya ya binadamu. na mazingira kwa ujumla.

Biashara ya matunda

9. Ni wajibu wa kila mfanyabiashara wa matunda kuhakikisha kuwa ana kifaa maalum cha kuhifadhia maganda au mabaki ya matunda.

Upulizaji dawa/ kuangamiza wadudu (fumigation)

10. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya upuliziaji dawa au biashara ya kuuwa wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila kuwa na cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na awe amelipia ada ya kibali kutoka Halmashauri kama ilivyoainishwa katika jedwali la kwanza la sheria ndogo hizi

Matengenezo ya magari, pikipiki, mitambo na kuegesha magari mabovu

11. (1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote;

(a) Kutengeneza gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo.

(b) Kuegesha magari mabovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi au barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo.

(c) Kufanya biashara ya kuosha gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo au kuruhusu eneo lake kutumika kwa shughuli za kuosha vyombo vya moto katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hizo bila kupata

kibali rasmi kutoka Halmashauri.

Udhibiti wa ubebaji kokoto, mawe na mchanga

12 1 Mtu yeyote atakayesafirisha mawe, mchanga au kokoto katika eneo la Halmashauri atahakikisha kuwa chombo anachotumia kusafirisha kimefunikwa ili kuzuia kumwagika na kuchafua mazingira.

2 Mtu yeyote hataruhusiwa kuchimba madini ya Ujenzi bila kuwa na kibali cha madini

Ufuaji wa nguo

13 Ni wajibu kwa mtu yeyote anayefanya biashara ya kufua nguo kupata hati ya usafi kabla ya kuanza biashara hiyo.

USIMAMIZI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kulinda na kutunza vyanzo vya maji

14 (1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa;

(a) kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(b) kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yoyote atakayeharibu chanzo cha maji, kuchafua chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

(c) kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya kitaalamu.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote: -

(a) kunawa, kuoga au kufulia nguo au kunywesha mifugo karibu au kwenye chanzo cha maji kama vile chemchem, kisima au chanzo kingine chochote cha maji au kunywesha mifugo

kwenye chanzo.

(b) kujenga boma la mifugo karibu au kuruhusu mkojo au maji machafu kuelekea kwenye au karibu na chanzo cha maji kwa matumizi ya binadamu.

(c) kufuga mifugo ya aina yoyote bila kibali cha Halmashauri; au kuacha mifugo au kusababisha mifugo kuzurura hovyo mitaani; barabarani au kuchungwa kwenye eneo lolote lisiloruhusiwa.

(d) kuanzisha na kufanya shughuli za aina yoyote ndani ya mita 60 katika maeneo yote oevu na chepechepe.

(e) kulima, kukata miti, kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 toka vyanzo vya maji au kujenga, kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(f) kumiliki eneo la chanzo cha maji cha asili isipokuwa Halmashauri.

(g) kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye Mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemchemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai.

(h) kuunganisha maji ya mvua na maji taka au kutapisha choo na kutiririsha vinyesi vya mifugo au binadamu kwenye chanzo cha maji au mfereji wa maji ya mvua.

(i) kuweka kitu chochote chenye sumu kwenye chanzo cha maji ambayo yanatumiwa na

binadamu au kiumbe chochote chenye uhai.

Kuchoma au kusababisha moto

15.(1) Ni marufuku kwa mtu yoyote: -

(a) kuchoma moto kwa namna yoyote ile katika eneo la Halmashauri;

(b) kuchoma moto taka ndani ya eneo la Halmashauri; au

(c) kuandaa shamba au kusafisha eneo lolote kwa njia ya kuchoma moto

2. Iwapo moto mkubwa utatokea katika eneo la Halmashauri, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyozoelekea na kuhamasisha wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo.

3. Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo na kama atashindwa kushiriki katika zoezi la kuzima moto bila sababu za msingi atakuwa ametenda kosa.

Uchafuzi wa anga hewa kwa moshi

16. Ni marufuku kwa mtu yoyote, mfanyabiashara, hospitali, taasisi, kaya, jengo au shughuli za viwanda kuchafua anga hewa “Air pollution” kwa kuachilia moshi angani unaoweza kuleta madhara kwa binadamu, mimea na viumbe hai.

Ukataji miti

17. (1) Ni marufuku kwa mtu yoyote kukata miti katika eneo la Halmashauri kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali.

(2) Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalumu ambao ni rasilimali ya Taifa.

(4) Mtu yoyote anaetaka kuvuna miti kwa ajili ya

kuchoma mkaa, mbao au kuni atatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kazi hiyo na atatakiwa kulipa ada ijulikanayo kama ada ya uchafuzi wa mazingira kwa kiwango kilichoainishwa kwenye Jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kupanda miti

18. (1) (a) Ni wajibu wa kila mkazi wa Halmashauri kupanda na kutunza miti katika eneo lake, makazi yake au shamba au mashamba anayoyamiliki.

(b) Kila mmiliki wa jengo la makazi au biashara atawajibika kutunza na kupanda miti katika eneo hilo kama inavyofafanuliwa katika Jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi.

2. Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata miti isipokuwa kwa kibali Manispaa

Uhifadhi na utunzaji Bustani za Halmashauri

19. Ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya biashara yeyote au kujenga chochote katika eneo la Bustani zote za Halmashauri.

Ushirikishaji wa jamii katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira

20. Mkurugenzi anaweza kutoa kibali kwa mtu yeyote, taasisi, kikundi binafsi au asasi ya kiraia, ndani ya Halmashauri katika ngazi ya Mtaa, Kata au Wilaya katika kuboresha bustani, eneo la wazi, kusimamia uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Tathimini ya athari kwa mazingira na jamii

21. (1) Miradi yote inayotekelezwa ndani ya Halmashauri haitaendelezwa bila kufanyiwa tathmini ya athari ya mazingira.

(2) Kila mpendekezaji wa mradi atawajibika kulipa Halmashauri asilimia kumi (10%) ya gharama ya tathimini ya athari za mazingira kama ada ya ukaguzi na usimamizi wa mradi husika.

Udhibiti wa kelele kwa shughuli mbalimbali za

22. Mtu yeyote haruhusiwi kusababisha au kufungulia kwa kelele kupita kiasi iwe muziki, kelele za kiwanda, jenereta au kitu kingine chochote (sound pollution) bila

kijamii kupata kibali cha Afisa Mwidhiniwa.

Makosa yanayotokana na uharibifu wa misitu

23. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa: -

(a) atachoma au kusababisha moto misitu bila ya kibali;

(b) atashindwa kushiriki katika kuzima moto:

(c) atavuna mazao ya miti katika misitu iliyohifadhiwa bila kibali;

(d) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali;

(e) atafyeka nyasi, kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali;

(f) atachunga mifugo kwenye eneo lolote lililopandwa miti au misitu iliyohifadhiwa kama bustani ya mtu;

(g) atakata miti au kuchungia mifugo kwenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kinga upepo;

(h) atabandua magome ya miti kwa ajili ya kueneza vilindo, mzinga na vitu vingine bila ya kuwa na vibali; au

(i) atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

SEHEMU YA NNE
USIMAMIZI WA AFYA YA MAZINGIRA

Usalama wa maji ya kunywa.

24. Ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama kwa kuyachemsha bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji.

Usalama wa maji ya visima

25. Ni wajibu wa kila mmiliki wa kisima kuhakikisha maji ya kisima yamepimwa ili yawe salama kwa matumizi.

Utengenezaji, na uuzaji vyakula.

26. Ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za afya na amepata kibali kutoka kwa Afisa Afya wa Halmashauri.

Uuzaji vyakula vilivyopikwa.

27. Ni wajibu wa kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa kuhakikisha kwamba vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao au kioo kuzuia inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.

Usalama wa vyakula.

28. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini, vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza.

(2) Ni marufuku kupanga vyakula nje ya duka la vyakula.

Uzuiaji wa shughuli mbalimbali wakati wa Magonjwa ya mlipuko

29. Afisa Mwidhiniwa anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.

Ukamataji wakati wa zuio

30. (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kumkamata mtu yeyote ambaye atakaidi amri ya zuio la kufanyika kwa shughuli ya uuzaji wa vyakula wakati wa magonjwa ya mlipuko.

(2) Endapo mtu aliyekamatwa alikuwa anauza vyakula ambavyo vinaharibika kwa haraka Halmashauri itaharibu vyakula hivyo.

(3) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1) na (2), endapo vyakula vilivyokamatwa vitakuwa haviharibiki kwa haraka Halmashauri itakuwa na jukumu la kuvihifadhi hadi mwisho wa amri ya zuio.

(4) Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa kwa uzembe wa Afisa wa Halmashauri.

Machinjio na maduka ya nyama

31.(1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama kuhakikisha kwamba duka lake;

(a) ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa kuwekwa sakafuni na ukutani marumaru nyeupe hadi urefu wa futi 6 kutoka usawa wa sakafu,

(b) lina maji safi, na misumeno ya kukatia nyama;

(c) lina kabati ya vioo na jokofu la kuhifadhia nyama na sehemu za mizani;

(d) lina pipa la kuhifadhia taka taka;

(e) lina mavazi maalum kwa ajili ya kuendeshea biashara ikiwemo aproni, mabuti meupe na kofia

(2) Muuzaji yeyote wa nyama atatakiwa kuvaa vazi jeupe pamoja na aproni nyeupe na sharti awe anapima afya kila baada ya miezi sita;

Kuchinja na kuuza nyama mahali pasiporuhusiwa

32. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyokuwa machinjio au maduka ya nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri.

Uendeshaji wa biashara ya Nyumba za kulala wageni na Hosteli

33. (1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba za kulala wageni, hosteli au nyumba za biashara kuhakikisha anapata kibali kutoka Halmashauri kabla hajaanza biashara.

(2) Endapo mmiliki hajakidhi masharti ya kiafya Halmashauri inaweza kuzuia kibali cha kuendesha biashara ya Nyumba za kulala wageni au hosteli mpaka hapo mmiliki atakapokuwa amekidhi masharti yaliyotolewa na Halmashauri.

Mahitaji ya nyumba ya wageni na Hosteli

34. Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, mgahawa, Hoteli na Hosteli kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa katika majengo hayo kuna; -

(a) mwanga na hewa ya kutosha;

(b) nafasi na vifaa (samani) za kutosha;
(c) mfumo wa uondoshaji wa maji taka na taka ngumu wa kuaminika;
(d) usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;
(e) vyoo na mabafu kwa jinsia zote;
(f) vifaa vya zima moto;
(g) tanki la kuhifadhia maji safi;
(h) Vyoo na bafu vilivyosakafiwa kwa vigae au marumaru na kuta zake zimewekwa vigae kiasi cha futi sita kutoka usawa wa sakafu.
(i) kuwa na jozi zaidi mbili za mashuka, foronya za mito na magodoro kwa kila kitanda na ziwe na rangi isiyoficha uchafu;
(j) kuwepo na sehemu maalumu ya kufulia na kuanikia nguo; na
(k) stoo na chumba cha kubadilishia nguo kwa ajili ya wafanyakazi

Upimaji wa afya

35.(1) Ni wajibu wa kila Mfanyakazi wa hoteli, gereji, saluni, kiwanda, wazoa taka, vyoo vya umma, mgahawa, baa, bucha sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, wafagiaji wa barabara na duka la kuuzia pombe kupima afya katika vituo vya Serikali au vituo vya afya vilivyoteuliwa na Halmashauri kila baada ya miezi sita.

(2) Ada ya kupima afya itakuwa kiasi cha shilingi elfu tano (5,000/=) kwa kila miezi sita.

Uwezo wa kukagua

36. (1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote muda wowote wakati wa saa za kazi na wakati wowote inapotakiwa kufanyika kwa ukaguzi maalumu kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Kufungwa kwa jengo la biashara lisilokidhi masharti ya afya

37. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.

Ada ya ukaguzi wa afya

38. Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya kiasi

cha shilingi elfu hamsini (50,000/=) ambayo italipwa kila mwaka kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara.

Muda wa kulipa ada

39. (1) Ada ya ukaguzi wa afya italipwa kila mwanzo wa mwaka wa fedha wa Halmashauri yaani mwezi Julai.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa ada katika kipindi cha miezi miwili baada ya mwaka wa fedha kuanza atawajibika kulipa kiwango hicho pamoja na adhabu ya asilimia hamsini ya kiwango anachodaiwa.

SEHEMU YA TANO
UDHIBITI TAKA NGUMU

Udhibiti utupaji wa taka

40. (1) Ni marufuku kutupa taka hovyo katika maeneo ya makazi, biashara, mifereji ya maji ya mvua, hifadhi ya barabara au mahali popote pasipotengwa kwa ajili ya kutupa taka.

(2) Ni marufuku kwa watumiaji wa vyombo vya usafiri binafsi au vya umma kutupa taka nje ya vyombo wanavyotumia na taka zote zitawekwa kwenye chombo cha kuhifadhia taka kilichomo kwenye chombo husika.

(3) Ni wajibu wa mtu yeyote au mkazi kuhakikisha kwamba anatupa uchafu au taka katika vyombo maalum vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalum yaliyotengwa.

Wajibu wa kuwa na pipa la taka

41 (1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara kuhakikisha kuwa ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili kuhifadhia taka ngumu kabla hazijachukuliwa kwa ajili ya kwenda kutupwa katika eneo lilotengwa kwa ajili ya kuhifadhi taka.

(2) Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara kuhakikisha kuwa ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili kuhifadhia taka ngumu na kinatumika kwa kazi hiyo kukitunza na

kukilinda.

(3) Ni wajibu wa kila mkazi au mtu yoyote kutunza na kuhifadhi vyombo vya kuhifadhia taka vinavyowekwa na Halmashauri.

Uanzishwaji wa Vikundi Jamii (CBOs)

42. Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa Vikundi Jamii (CBOs) na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Uhifadhi maji taka

43 (1) Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kufungulia na kutiririsha maji taka au kinyesi kutoka chooni au sehemu yoyote wakati wa mvua au wakati wowote kwenye mifereji ya maji ya mvua, mabonde au maji yanayotembea au sehemu nyingine yoyote isiyoruhusiwa.

Kutiririsha maji taka

44. Ni marufuku kutiririsha au kuelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni, baada ya kufua au kuosha vyombo kwenda sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhi maji taka.

Taka za viwanda

45. (1) Ni marufuku kwa kiwanda chochote kutoa au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu au harufu mbaya, vumbi au kelele na kusababisha kero kwa wakazi wa eneo la Halmashauri.

(2) Ni wajibu wa kila mwenye kiwanda kuhakikisha kuwa taka kama vile vumbi, maganda, moshi na takataka nyingine zinazoweza kuleta kero au adha kwa

ujumla haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe wengine hai.

Kaya au Jengo la biashaara kulipa Ada taka

46. (1) Halmashauri itatoza ada ya uzoaji taka kutoka kwa kila kaya, mwenye jengo la biashara au taasisi yoyote ile.

(2) Ada ya kila mwezi italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika na italipwa kwa Afisa Mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo kwa njia ya kieletroniki yatakayolipwa na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka.

(3) Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 16 cha Sheria Ndogo hizi ni marufuku kwa mtu yeyote, kampuni, wakala au taasisi kuendesha shughuli za uchomaji wa taka hatarishi bila ya kupata kibali kutoka Halmashauri.

SEHEMU YA SITA
UJENZI NA MATUMIZI YA VYOO

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

47. (1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi, imara kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo.

(2) Kuweka sehemu maalum ya kunawia mikono ikiwa na maji safi na sabuni maalum ya kimiminika.

Umbali wa kujenga choo

48. Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa mita sitini (60) kutoka chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya Nyumbani.

Vyoo vya umma

49. (1) Halmashauri inaweza kujenga Choo cha Umma au kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya Umma (Public toilet) katika maeneo ambayo Halmashauri itaona inafaa.

(2) Vyoo vitakavyojengwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi vitatakiwa kiwe cha kudumu na: -

(a) matundu yasiyopungua mawili (2) kwa wanawake na mawili (2) kwa wanaume.

(b) mfumo madhubuti wa maji na uwepo wa maji ya kutosha yaliyo safi na salama,

(c) kuwepo na chombo cha kuhifadhia maji ya akiba

(d) kuwepo kwa bafu ya wanaume na wanawake

(e) kuwepo na chumba maalumu cha Kuvutia sigara

(f) kuwepo na sehemu ya haja ndogo kwa wanaume

(g) kuwepo na chombo maalumu chenye mfuniko cha kuhifadhia taka zisizoweza kusukumwa na maji.

Vyoo vya muda katika mikusanyiko

50. Ni wajibu wa mtu yeyote, kikundi au taasisi yenye lengo la kukusanya watu kwa madhumuni ya mkutano, sherehe au mkusanyiko wowote kuweka au kujenga vyoo vya muda endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu na atatakiwa kuomba idhini kutoka Halmashauri

Vyoo katika majengo ya biashara

51. Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo vyenye viwango

vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hizi kwa ajili ya matumizi ya wateja wake kwa kuzingatia jinsi zote

Ilani ya kujenga au kurekebisha choo

52. Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo.

Kufungwa kwa jengo

53. Bila kuathiri masharti ya kifungu cha (52) Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa shughuli za makazi au biashara hadi hapo hali hiyo itakapokuwa imerekebishwa.

Ilani ya kuondoa kero

54. (1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo ndani ya muda kadri ambavyo ataona inafaa.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.

Eneo maalumu la uvutaji sigara

55. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvuta sigara kwenye eneo la wazi au kwenye mikusanyiko ya watu.

(2) Kila mwenye jengo la biashara za Baa, Hoteli, mgahawa, kumbi za starehe, viwanja vya michezo na burudani, Ofisi za umma na binafsi anatakiwa kutenga eneo maalum la kuvutia sigara na kuweka chombo cha kuhifadhia majivu na vichungi vya

sigara

Ukaguzi wa Afya

56. Halmashauri kupitia Afisa afya Mazingira itafanya ukaguzi wa afya kwenye maeneo yote ya makazi, biashara au shughuli yoyote yaliyopo katika eneo la Halmashauri.

Makosa

57. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo;

(a) atamzuia au kujaribu kumzuia au atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) atamwaga au kutupa taka barabarani, mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni, au mahali popote hadharani au katika eneo lolote lisiloruhusiwa;

(c) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;

(d) atatiririsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;

(e) ataosha magari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;

(f) atapika vyakula pembezoni mwa barabara au nje ya majengo mengine.

(g) atauza vyakula maeneo yasiyo

rasmi na kushindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;

(h) atafanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo, katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(i) atavuta Sigara hadharani au mahali pa jumuiya au kwenye vyombo vya usafiri

(j) atatema mate hovyo au kutema mate barabarani au mahali pa jumuiya.

(k) ataacha nyumba anayoishi au kumiliki au kufanyia shughuli zake katika hali ya uchafu yenye kuleta kero au chukizo.

(l) ataacha chombo cha Usafiri katika hali ya uchafu.

(m) ataendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(n) ataanzisha au kufungua karakana katika majengo, majumba au maeneo ya makazi;

(o) ataenda haja ndogo au kubwa hovyo barabarani, uchochoroni, upenuni au mahali popote ambapo siyo

chooni; au

(p) atafanya biashara ya kuosha gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo au kuruhusu eneo lake kutumika kwa shughuli za kuosha vyombo vya moto katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hizo bila kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri;

Kufifilisha Kosa

58 Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kiasi kisichozidi shilingi Laki Mbili (Tsh.200, 000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hizi,

Adhabu

59 Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia kama hakuna adhabu maalumu iliyoainishwa katika kifungu kilichokiukwa atatozwa faini isiyozidi shilingi Laki Tatu (300,000) au kutumikia kifungo kisichozidi miezi Kumi na Mbili (12) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Tangazo serikali na. 495 (linaendelea)

JEDWALI LA KWANZA

(Limetungwa chini ya kifungu cha 5)

Ada ya Uzoaji wa Taka

Na	Aina ya mzalishaji taka	Kiwango cha ada kwa mwezi (Tsh)
1	Nyumba za makazi (Kwa kaya)	3,000 hadi 10,000
2	Nyumba ya makazi ghorofa moja	20,000
3	Nyumba za makazi zaidi ya ghorofa moja	30,000
4	Nyumba kubwa ya pekee (Bungalow)	30,000
5	Nyumba ya pekee yenye nyumba za huduma (Villa)	50,000
6	Penthouse	50,000
7	Hostel (kwa chumba)	2,000
8	Nyumba ya kulala wageni (Guest house)	50,000
	OFISI	
	Ofisi - 1 – 10 wafanyakazi	50,000
	Ofisi – 11 – 50 wafanyakazi	100,000
	Ofisi – 51 – 100 wafanyakazi	200,000
	Ofisi – 101 – zaidi ya wafanyakazi	400,000
9	Tawi la Benki ya biashara	150,000
10	Duka la kubadilishia fedha	100,000
11	Ofisi za ATM	100,000
12	Ofisi za luku (Tanesco)	100,000
13	Ofisi za luku(wakala)	50,000
14	Mawakala wa fedha kwa mitandao ya simu na benki	30,000
	VYAKULA NA VINYWAJI	
15	Sehemu ya kutengenezea chai na vitafunwa (tearoom, snacks &soft drinks)	20,000
16	Cafe/Restaurant (food/snacks & soft drinks)	
	Hadi viti 20	100,000
	Zaidi ya viti 20	300,000
17	Duka la vyakula na vinywaji (Grocery)	15,000
18	Baa (pombe, vinywaji baridi na vitafunwa)	30,000
19	Mama na baba lishe	15,000
20	Taka zinazotokana na Biashara ya Mgahawa wa nje ya Majengo (Open Air Restraurant)	100,000
21	Vibanda vya chips	15,000
22	Baa na mgahawa/jiko	
	Hadi viti 20	50,000
	Zaidi ya viti 20	100,000
23	Baa na nyumba ya kulala wageni (Bar&Guest house)	100,000
24	Baa, nyumba ya wageni na Ukumbi wa starehe	200,000
25	Baa na ukumbi wa starehe	150,000
26	Baa, Ukumbi wa starehe na mgahawa	200,000
27	Ukumbi wa starehe	100,000
	Watu 01 hadi 300	150,000

Tangazo serikali na. 495 (linaendelea)

	Watu 301hadi750	300,000
	Watu750.hadi2000	400,000
	Zaidi ya watu 2000	500,000
28	Duka la kuuza *Ice Cream*	20,000
29	HOTEL&LODGE	
	Hadi vyumba 10	150,000
	Vyumba 11- 20	250,000
	Vyumba 21- 30	350,000
	Vyumba 31- 40	450,000
	Vyumba 41- 50	550,000
	Vyumba 51- 70	650,000
	Vyumba 71- 100	750,000
	Zaidi ya vyumba 100	1,000,000
30	Bucha ya nyama na /au samaki wabichi	10,000
31	Vyakula/bidhaa mchanganyiko	30,000
32	Duka la nguo	20,000
33	Vifaa vya umeme au simu (Electronic phone, phone accessories and electrical appliances)	40,000
34	Vifaa vya ujenzi Hardware/ Machinery	80,000
35	Vitabu/ Shajala (Stationaries)	20,000
36	Urembo/ Vipodozi	20,000
37	Duka la Samani (Furniture and Machinery)	40,000
38	Vinywaji na Pombe Kali (beverages and liquor stores)	30,000
39	Taka zinazotokana na ghala la kuhifadhia bidhaa (Store)	50,000
40	Vipuri na Vifaa (Spare parts and tools)	20,000
41	Duka la vifaa chakula	20,000
42	Fundi Seremala	30,000
43	Karakana ya Chuma (Metal W/ shops)	30,000
44	Karakana ya Magari (Motor Garage)	50,000
45	Sonara na uhunzi wa vito (Jewerly and Black Smith)	15,000
46	Shughuli za Vioo (Glass Works)/ Shughuli za Alminium	50,000
47	Mchapishaji (printing)	100,000
48	Store	40,000
49	Mashine ya mbao kwa ujazo wa mita moja saw mill per m^3	15,000
50	Kwa tani moja ya taka kwa ujazo mkubwa	25,000
51	Kwa ujazo wa mita moja cubic meter	25,000
52	Umeme na Matengenezo ya elektroniki (Electronical anad Electronic repair)	25,000
53	Magurudumu na matengenezo	20,000
54	Fundi cherehani	20,000
55	Seremala	20,000
56	Fundi viatu (cobler/ Shoe repair)	5,000
57	Saluni ya nywele	20,000
58	Dobi and dry cleaner	10,000
59	Genge kwa meza moja	5,000
60	Biashara ya juisi ya miwa	40,000
61(a)	Wauza matunda na juisi nyinginezo	20,000
61(b)	Wafanyabiashara wadogo wasio na maeneo maalum.	500 kwa siku

Tangazo serikali na. 495 (linaendelea)

62	Huduma za Intenet	10,000
63	Duka la dawa baridi	20,000
64	Pharmacy	50,000
65	Duka la dawa rejareja (Retail)	30,000
66	Duka la vifaa vya maabara	30,000
67	Maabara ya Vipimo	20,000
68	Zahanati	50,000
69	Kituo cha Afya	70,000
70	Madawa asilia	30,000
71	Hospitali	100,000
72	Kliniki/Herbalist	50,000
73	Hospitali ya Rufaa	400,000
74	Kituo cha kulelea watoto, shule ya sekondari, shule ya msingi na vyuo	
	Hadi Wanafunzi 200	100,000
	Wanafunzi 201- 500	200,000
	Wanafunzi 501-1,000	300,000
	Zaidi ya wanafunzi 1000	500,000
75	Kituo kikubwa cha mafuta (zaidi ya Pump 6) na service staton	200,000
76	Kituo kidogo cha mafuta (pump 1-5) na service station	150,000
77	Kituo cha mafuta bila service station	100,000
78	Kituo cha mafuta ya taa	20,000
79	Biashara ya kuuza/kufatulia tofali	50,000
80	Kituo cha Kuuzia gesi	50,000
81	Kibanda cha Kuuzia mkaa (Kikubwa zaidi ya gunia 10)	40,000
82	Kibanda cha Kuuzia Mkaa (Kidogo gunia 1- 10)	30,000
83	Msikiti au Kanisa bila ya kuwa na shughuli nyingine za Kibiashara	30,000
84	Msikiti au Kanisa ukiwa na shughuli nyingine za Kibiashara	100,000
	HUDUMA NYINGINEZO	
85	Jumba la Starehe/ Klabu/cassino/night clubs	250,000
86	Ofisi za ulinzi	20,000
87	Tax kwa siku	500
88	Ofisi za tiketi za mabasi na kuhifadhi mizigo	50,000
89	Daladala kwa siku	1,000
90	Lori la mizigo	5,000
91	Minara ya simu na mawasiliano mengine	30,000
92	Kituo cha transformer ya umeme (Electric transformer stations)	100,000
	TAKA ZENYE UJAZO MKUBWA (BULKY AND BUNDLE WASTE)	
93	Taka za bustani kwa mita mraba moja	25,000
94	Taka za ngmu toka viwandani	400,000 kwa tripu
95	Taka za masoko kwa tani	25,000
96	Ghala (Godown)	100,000
97	Duka la vifaa vya muziki	40,000
98	Duka la CD na cassette	20,000
99	Bahati Nasibu	20,000
100	Taka za Biashara kwa tripu	400,000

Tangazo serikali na. 495 (linaendelea)

	(Super market hyper market na nyinginezo)	
101	Taka za uvunjaji wa jengo kwa tani moja (demolition debris per tonne)	50,000
102	Kituo cha kuchakata taka (waste recycling center)	60,000

JEDWALI LA PILI.

(Limetungwa chini ya Kifungu cha 17(4))

ADA YA UCHAFUZI WA MAZINGIRA

(a) Mkaa shilingi elfu moja (1,000) kwa gunia
(b) Mbao shilingi elfu tano (5,000) kwa kila ujazo wa mita (1M3)
(c) Kuni shilingi elfu tatu (3,000) kwa kila ujazo wa mita moja (1M3)

JEDWALI LA TATU.

(Limetungwa chini ya Kifungu cha 18(1)(b))

UPANDAJI MITI

Ujazo wa Juu	Miti isiyo pungua 2
Ujazo wa kati	Miti isiyo pungua 4
Ujazo wa chini	Miti isiyo pungua 5

Tangazo serikali na. 495 (linaendelea)

JEDWALI LA NNE

HATI YA KUFIFISHA KOSA

(Limetungwa kwa chini ya kifungu cha 58)

Mimi ……. nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya ……..……ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwamba mnamo tarehe ……. ya Mwezi……..Mwaka……nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi za Afya na Usimamizi wa Mazingira za Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo za mwaka 2022.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa niko tayari kulipa kiasi cha shilingi,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,kama faini ninayodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……. ya Mwezi……. Mwaka…….

Jina……...…….

Saini……..……

Mbele ya…….……...

Cheo…….……

Saini……...……

Tarehe……...…….

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 13 Mwezi Agost, 2021

BEATRICE R DOMINIC
Mkurugenzi
Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo

JAFFARY JUMA NYAIGESA
Mstahiki Meya,
Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo

L.S

NAKUBALI;

DODOMA
2 Julai, 2022

INNOCENT L. BASHUNGWA (MB),
Waziri wa Nchi or - Tamisemi.